AL-HABIB MUHAMMAD BIN HASSAN AL-NADHIRY

(MWENYE KARAMA)

1355 – 1441 H

1936 – 2020 CE

AL-FAQEER

YAAKUB ABDULHAMID SHEIKH

1441 AH / 2020 CE

IMEKUSANYWA NA KUANDIKWA NA

AL-FAQEER, YAAKUB ABDULHAMID SHEIKH

IMESAHIHISHWA NA:

USTADH ABDULRAZAQ SALEH
SAYYID UMAR M. ABRAR AL-NADHIRY
SAYYID MUHAMMAD (BAHSAN) AIDARUS NOOR AL-NADHIRY

Barua pepe: yaakub.ahmed@gmail.com

Kwa masihihisho ya upungufu au ziyada tafadhali wasiliana na anwani iliyotajwa.

Al-Habib Muhammad bin Hassan Al-Nadhiry
(Mwenye Karama)

KWA JINA LA MWENYE-EZZI-MNG'U, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

UTANGULIZI

Kila jinsi ya sifa njema anayestahiki kusifiwa ni Mwenye-Ezzi-Mng'u, Mola wa viumbe vyote. Na rehma na amani zimfikie aliye mtukufu wa daraja, Bwana wetu Muhammad pamoja na Aali zake na Maswahaba zake.

Karibuni katika toleo hili la kwanza la tarikh ya Mwenye Karama. Lengo na madhumuni ya makala haya ni kumuarifisha Mwenye Karama ili watu wapate kuijua tarikhi yake na waweze kuiga mema aloyafanya, pamoja na kujua kazi kubwa aliofanya katika kuelimisha ummah.

Tumehimizwa kuwaiga waja wema hata kama hatutoweza kufanya amali au kufika maqamu waliofika wao. Na anasema Mwenye-Ezzi-Mng'u katika Qur'an takatifu mwisho wa aya ya 176 katika Suratul A'araf;

"..Basi simulia hadith, huenda wakatafakari."

Twamuomba Mola Subhanahu wa Ta'ala atunufaishe na ilimu na baraka za bwana huyu. Amin, Wa billah Tawfiq.

Al-Faqeer
Yaakub Abdulhamid Sheikh

AALNADHIRY

Aal Nadhiry ni mlango wa masharifu wa Ba Alawy wa kutoka Hadhramaut. Ukoo wa Al-Nadhiry unatokana na Sayyid Muhammad Al-Nadhiry bin Abdallah bin Umar Ahmarul Uyuun bin Abdulrahman bin Ahmad bin Alwy bin Al-Faqih Ahmad[1] bin Abdulrahman bin Alwy[2] Am'ul Faqihul Muqaddam.

Sayyid Muhammad Al-Nadhiry alizaliwa mji wa Tarim huko Hadhramaut, Yemen mnamo mwaka 739 AH.
Sababu ya kupewa laqab ya "Al-Nadhir" ni sababu alikuwa mtu mtanashati na mzuri wa sura na tabia.

Aal Nadhiry pamoja na Aal Ba Faraj ndio wa mwanzo miongoni mwa Sada Alawiyyin waliogura kutoka Yemen kuja Afrika ya Mashariki[3]. Mwanzo wa kugura kwao walipitia Somalia kisha wakahamia Kenya halafu wakatawanyika kuelekea Unguja na Comoro na nchi nyenginezo. Aliyetangulia kuhama kutoka Tarim kuja nchi za afrika ya mashariki ni Sayyid Ahmad bin Umar[4] (aliyepewa laqab ya Ahmarul Uyuun) bin Muhammad al-Nadhiry. Sayyid Ahmad alihama mji wa Tarim Al-Ghannaa ulioko Hadhramaut akaelekea kijiji kiitwacho

---

[1] Alifariki 720H
[2] Alifariki 613H
[3] Tizama kitabu Haadhir Aalam Islamiy (The New World of Islam) Mj 3 Uk 183 kilichoandikwa na Lothrop Stoddard na kufanyiwa tahqiq na Amir Shakib Arslan
[4] Sayyid Umar bin Muhammad Al-nadhiry alifariki siku ya Ashuraa 1017H na alizikwa karibu na babake; Muhamaad Al-Nadhiry hapo Tarim.

Mirbat katika mji wa Dhafar takriban mnamo mwaka wa 1000H.

Katika mji wa Dhafar, Sayyid Ahmad aliruzukiwa kijana aliyemwita Alwy[5]. Sayyid Ahmad akahama nchi na mwanawe Alwy wakaelekea mji wa Mogadishu katika nchi ya Somalia. Waliwasili hapo siku ya alkhamisi tarehe 27, Rajab, 1003H. Sayyid Ahmad alifunga ndoa hapo Mogadishu na akajaaliwa kijana aliyemwita Abubakar[6]. Baada ya kukaa hapo kwa muda usiokuwa mrefu akahama tena na safari hii akaelekea katika kijiji cha Pate moja wapo katika vijimbo vya Lamu katika nchi ya Kenya. Sayyid Ahmad alifariki Pate mnamo mwaka wa 1027H na akazikwa mbele ya msikiti wa jaamia alokuwa ameujenga.

Kutokana na kizazi cha watoto wawili wa Sayyid Ahmad bin Umar (Ahmarul Uyuun) bin Muhammad al-Nadhiry kukatoka tandu tofauti tofauti na wakawa na laqab nyenginezo.

Waliotokana na Alwy bin Ahmad Al-Nadhiry;

1. Aal Mwenye Ahmad
2. Aal Ahmad Magalo

Waliotokana na Abubakar bin Ahmad Al-Nadhiry

1. Aal Sharif Noor Ali

---

[5] Mamake Alwy alikuwa akiitwa Aisha bint Abdallah bin Makki bin Muhammad bin Sheikh Fadhil bin Abdallah Ba Fadhil.

[6] Mamake Abubakar alikuwa akiitwa Fatma bint Ahmad DirDir

2. Aal Sharif Muhammad Abu

Idadi ya Aal Nadhiry ni wengi mno na wameenea katika nchi za Hijaz, Yemen na Afrika ya Mashariki, hasa nchi ya Unguja, Somalia katika miji ya Mogadishu, Marka na Barawa na Kenya katika visiwa vya Lamu na Mombasa.

AL-HABIB MUHAMMAD BIN HASSAN AL-NADHIRY, MWENYE KARAMA

JINA NA NASABA YAKE

Al-Habib Muhammad bin Hassan bin Ahmad bin Hassan bin Nur bin Abubakar bin Muhammad bin Aidarus bin Abdullah bin Abubakar bin Ahmad bin Umar bin Muhammad (Al-Nadhiry) bin Abdullah bin Alwy bin Umar (Ahmarul Uyuun) bin Abdulrahman (Swahib Masjid Babtweyn) bin Ahmad bin Alwy bin Ahmad bin Abdulrahman bin Alwy (Ammul Faqiih) bin Muhammad bin Ali Khaal' Qasam bin Alawy bin Muhammad bin Alawy bin Ubaidillah bin Ahmad Al-Muhajir-ila-Llaah bin Isa An-Naqiib bin Muhammad Jamaluddin bin Ali Al-Ureidhy bin Ja'far As-Swadiq bin Muhammad Al-Baaqir bin Ali Zeynul Aabidin bin Hussein As-Swibty (R.A) bin Al-Imam Ali bin Abi Twalib (R.A) na mamake akiwa ni As-Sayyida Fatimah Az-Zahraa (R.A), binti Rasulillah (Swalla-Llahu Aleyhi Wasallam)

Mwenye Karama, ambalo ndio jina maarufu la Al-Habib Muhammad bin Hassan Al-Nadhiry, alizaliwa mnamo mwaka wa 1355 H / 1936 CE katika kijiji cha Mbwajumwali, kisiwa cha Faza, moja wapo katika visiwa vya Lamu.
Mamake alikuwa akiitwa Khadija wa Shafii bin Athman[7] wa Siyu.

---

[7] Bwana Athman wa Siyu asli yake ni kutoka Barawa. Alihama Barawa akaja Chundwa na akaoa. Aliruzukiwa watoto wawili; Shafii na Hassan. Bwana Athman alijenga mskiti mkubwa hapo chundwa.

SHAJARA LA MWENYE KARAMA



KUPEWA LAQAB YA MWENYE KARAMA

Al-Habib Muhammad bin Hassan alipewa laqab hii ya "Mwenye Karama" kwa kiswa kilichotokea kwao Mbwajumwali. Safari moja nyumbani kwao kuliwaka moto, na moto ule ukaenea nyumba nzima. Ndani ya nyumba ile kulikuwa na nduguye mdogo, na ndipo Mwenye akaamua kuingia ili kuenda kumuokoa.

Alipoingia mle ndani, moto ukawa umeshika sasa nyumba nzima. Lakini Mwenye-Ezzi-Mung'u hawatupi waja wake, akawahifadhi na wakatoka salama.

Baada ya kiswa hiki, babuye akamwita "Mwenye Karama" (yaani aliyepewa Karama ya kuhifadhiwa na Mola wake.

MALEZI YAKE

Mwenye Karama alifiliwa na babake angali kijana. Jukumu la kumlea mwana likamshukia mama mzazi. Mama akasaidiana na babu; Bwana Shafii, wakamlea Mwenye kwa malezi mema hadi akafika umri wa kuweza kutafuta rizki yake mwenyewe. Maisha yalipoanza kuwa magumu pale Mbwajumwali, Mwenye akafunga safari kuelekea Mombasa.

KUHAMIA MOMBASA

Mwenye Karama alihamia mji wa Mombasa katika ujana wake, na akawa anajishughulisha na kazi mbali mbali ili kujikimu kimaisha. Hakuchagua kazi, alifanya kazi ya uhamali katika bandari ya Mombasa na kupaka rangi meli. Baadaye akafanya kazi ya kuuza vipuli, akawa analeta mali kutoka Unguja kwenye vikapu alivokuwa akibeba kichwani. Pia alifanya kazi ya kuuza mboga sokoni.

KUSOMA KWAKE

Mwenye Karama kando na kufanya kazi na kutafuta riziki ya halali pia hakuwacha mwendo wa wazee wake kutoka ukoo wa "Ba-Alawy", nayo ni twariqa ya kusoma na kutafuta ilimu popote pale na kwa hali yoyote ile. Alikuwa na hima pamoja na bidii ya hali ya juu katika nyanja hiyo. Alikuwa akitoka mtaa wa Kisauni kwa Miguu hadi mtaa wa Makadara katika Msikiti wa Mbaruku kwa lengo la kutafuta ilimu, akasoma na zikasomeka.



MASHEKHE ZAKE MWENYE KARAMA

AL-ALLAMAH SHEIKH MUHAMMAD BIN AHMAD BIN ALI AL-LAAMY AL-BEREKY (SHEIKH BEREKY)

Sheikh Bereky ndiye shekhe wake mkubwa na ndiye Sheikhu fat'hihi. Alisoma kwake kwa muda wa miaka thalathini na tatu.
Katika muda huu alisoma mengi sana lakini itoshe kuwa alinakili kitabu cha Minhaj Twalibiin cha Al-Imam Nawawy mara saba mbele yake (kunakili ni kusoma kitabu mwanzo mpaka mwisho), na ndiye aliyemuachia Darasa lake la Msikiti wa Azhar katika mtaa wa Kibokoni,

Sheikh Bereky alikuwa ndiye Shekhe wa Mombasa katika wakati wake, kwani hakuna Shekhe yeyote wa Mombasa wa zama zake isipokuwa amesoma kwake, hata Al-Imam Sayyid Muhammad al-Beidh alikuwa akikariri kila wakati huku akisema "Sheikh Bereky alifanya kazi kubwa sana ndani ya Mombasa, na hakuna mwanachuoni yeyote wa ki-Mombasa isipokuwa elimu yake yarudi kwake (Sheikh Bereky)", na hii ni kupitia hima na bidii alizo kuwa nazo katika kufunza.

Sheikh Bereky alizaliwa Lamu tarehe 20 Mfungo Sita 1328 A.H. sawia na tarehe 1st April 1910 CE

Waalimu wake Sheikh Bereky

1. Sheikh Abdalla bin Muhammad Al-Khatib
2. Sayyid Ahmad Badawy Jamalullayl
3. Sayyid Abdalla bin Ahmad Al-Ahdaly
4. Sh. Abdulmajid bin Zahran
5. Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui
6. Sheikh Ali bin Khalid Al-Laamy

Wanafunzi wa Sheikh Bereky:

1. Sayyid Abdulrahman bin Ahmad Badawy (Sharif Khitamy)



2. Sayyid Ahmad Badawy (Sharif Badawy wa Mwenye wa Nana)

3. Sheikh Abdulrahman Muhammad Al-Hatimy



4. Sheikh Ali Muhammad Mwinzagu

5. Maalim Shee bin Ibrahim

6. Sheikh Nassor Muhammad Al-Nahdy



Wengineo waliosoma kwa Sheikh Bereky ni

7. Shee Abdallah wa Shee Bakari
8. Sheikh Ali Gunda
9. Sheikh Goso bin Ibrahim

Na wengine wengi..

Sheikh Bereky alifariki jumanne tarehe 26 Rabiul Thani 1406 AH / 1986

AL-HABIB AHMAD MASH'HUR TWAHA AL-HADAD

SAYYID MUHAMMAD BIN AHMAD AR-RUDAINY (MWENYE MUADHAM)

AL-HABIB SAEED BIN ABDALLAH AL-BEIDH

AL-HABIB ALI BIN AHMAD BADAWY JAMALULLAYL

AL-HABIB ABDULRAHMAN BIN AHMAD BADAWY JAMALULLAYL (SHARIF KHITAMY)

Mwenye Karama alitabaruku kwake ilimu ya tiba

KATIKA HIKMA ZAKE

Mwenye Karama alikuwa akihudhuria darasa zilizokuwa zikiendeshwa na wanafunzi wake. Ada ya wanafunzi wakimaliza darasa ni kwenda kumuamkua Sheikh wao na kumuuliza iwapo darasa ilienda sawa sawa.

Siku moja, mwanafunzi alokuwa akiendesha darasa akateleza katika tafsiri. Darasa ilipoisha, akamwendea Mwenye kama ilivyo ada. Mwenye akamwambia maneno haya ili kumweleza kosa alilofanya; "… Nenda utizame tena vizuri darasa ya leo. Ukitwalii utaona mengi.." Hakuwa haraka kukosoa mtu hadharani.

Katika hikma zake, alikuwa hatolei wanafunzi au watu wake wakaribu ukali. Iwapo mtu hakumpita siku nyingi, atamuulizia na kumtolea udhru. Na pindi mtu yule akienda kumtizama, basi jambo la kwanza atakwambia ni "Jee?"

Neno hili moja "jee?" ndilo alokuwa akilitumia. Baada ya hapo basi huendelea na mazungumzo mengine.

KAZI ZAKE

Mwenye Karama alikuwa na juhudi kubwa katika kusomesha,bali alikuwa akisema kuwa “sioni udhru wowote wa kukosa Darasa,” na mara nyingine alikuwa hufika Msikitini huku amerowa kwa mvua al-haaswil asikose kusomesha darasa kabisa,na huu ndio uliokuwa mwenendo na kawaida yake mpake utu uzimani mwake na mpaka kufariki kwake Dunia.

Mwenye Karama alikuwa ni msomi mkubwa wa fani mbalimbali na aliyekusanya Mawaddi mbalimbali za lugha ya kiarabu na elimu ya Dini,lakini alivama zaidi katika somo la Fiqhi,somo ambalo amesomesha vitabu vikubwa sana ambavyo si yeyote awezae kuvisomesha kama “Attanbih cha Abuu Is’haq Ibrahim bin Ali bin Yusuf Al-Shiirazy na Alwajiiz cha Imam Ghazaaly”,mpaka kufikia baadhi ya watu kusikika wakisema kuwa “Mwenye Karama katika elimu ya Fiqhi,utadhania kuwa vile vitabu va Fiqhi vilichukuliwa vikachemshwa kisha yale maji akapewa yeye kuyanywa”,na hii ni kwa ufahamu wake mzuri wa somo hilo ambalo hutatiza wengi. Mwenye Karama alikuwa na darasa nyingi sana katika Misikiti tofauti na nyakati tofauti,na labda hapa tutaje ratiba yake ya kila siku pamoja na darasa zake,Mwenye Karama alikuwa akienda Msikitini wakati wa
Muadhini wa kwanza ambapo alikuwa na darasa kabla ya Swala ya Alfajiri katika Msikiti wa Nuur Bondeni,kisha baada ya Swala atoke awapatie maskini walioko nje ya

Msikiti sadaka,kisha arudi Msikitini asome Hizbu mpaka saa kumi na mbili unusu 6:30am,kisha asomeshe tena darasa mpaka saa moja na nusu 7:30am ndipo aswali Swala ya Ishraq na Dhuha, kisha atoke akatafuta riziki yake ya halali na alikuwa na kiduka chake kidogo akiuza mboga pale Marikiti,darasa hii ya Masjid Nuur aliianza katika miaka ya Thamanini mwisho mwisho na alidumu nayo mpaka ulipofungwa Msikiti Nuur kwa ajili ya marekebisho,kisha zile darasa za Msikitini akazigurishia nyumbani kwake kwa kuwa umri pia ulikuwa umeenda sana. Mwenye Karama alipogurisha zile darasa nyumbani kwake ziligawanyika mara tatu,kulikuwa na darasa Asubuhi,kabla ya Swala ya Adhuhuri na alikuwa na darasa nyingine baada ya Swala ya Alasiri mpaka saa kumi na moja unusu,na baada ya Magharibi alikuwa na darasa katika Msikiti wa Azhar Baghani,darasa ambayo alirithishwa na Shekhe lake “Sheikh Bereki” alipolemewa na maradhi na hapo ni katika mwaka wa 1983CE, na alidumu na darasa hiyo mpaka mwaka wa 2018 miaka 35 kisha kwa sababu za afya na utu uzima ndipo akasitisha darasa hiyo,pia alikuwa na darasa nyingine katika Msikiti Nuur darasa la Tafsiir baada ya Swala ya Alasiri kila siku katika mwezi wa Ramadhani.

KITAMBULISHO CHA ILIMU YAKE YA UTABIBU

MUSLIM WAKIL

Mwenye Karama ndiye aliyekuwa Wakili wa kwanza Muislamu Kenya katika Kaadhi's Court, yeye pamoja na rafiki yake waliosoma pamoja kwa Sheikh Bereki akiitwa Shaykh Abdul-Rahman bin Muhammad Al-Hatimy, na Shahada ya kufanya kazi hiyo alipewa na mwalimu wake Sheikh Bereki, na alimpendekeza kwa maneno haya, nanukuu:

"Ijulikane kwa kila mwenye kusoma hii barua, kwamba Sharif Muhammad bin Hassan amesoma ilimu ya Fiqhi na fani nyingi zenginezo kama vile Nahaw, Swarfa, Balaagha na Usuulul Fiqh na Mustalahil Hadith na Mantiq na Tafsir kwa Al-Al'lamah Sheikh Muhammad bin Ahmad al-Bereky na chini ya inaya yangu amefikia daraja ya kuweza kushughulika kibinfasi kuwa Muslim Wakil katika Mahkama ya Kadhi Kenya"

Mwisho wa nukuu

HAJI M. S. MOHIDIN & SONS

IMPORTERS & EXPORTERS

GENERAL MERCHANTS & COMMISSION AGENTS

BANKERS:
KENYA COMMERCIAL
BANK LTD. MOMBASA

Telephone No. 24471,
P. O. Box No. 81322

MOMBASA
(KENYA)

197

ليعلم كل من يقف على هذا بأن شريف
محمد بن حسن تلقى علم الفقه وفنونا أخر
من النحو والصرف والبلاغة وأصول الفقه
ومصطلح الحديث والمنطق والتفسير من
العلامة الشيخ محمد بن احمد البركي وتحت
عنايته وقد بلغ درجة استطاع بالاشتغال
لنفسه كمسلم وكيل في محاكم القضاة في كينيا

وكتبه عبد الرحمن محمد الحلاق

محمد بن احمد البركي

COLONY AND PROTECTORATE OF KENYA

HER MAJESTY'S SUPREME COURT OF KENYA

LICENSED VAKIL'S CERTIFICATE

(Issued under section 22 of the Advocates Ordinance, No. 55 of 1949)

This is to certify that .....SHARIFF MOHAMED BIN HASSAN.....

.....

is licensed to practise as a Vakil in the Subordinate Native Courts of the Province of

.....COAST.....

This licence, unless cancelled, shall remain in force for one year from the

.....11th September, 1962.....

Given under my hand and the Seal of the Supreme Court of Kenya.....11th.....

day of .....September..... in the year of Our Lord One Thousand Nine Hundred

and .....Sixty-two..... at .....NAIROBI.....

.....

Ag. *Chief Justice,*
Supreme Court of Kenya.

G.P.K. 2685—500—10/59

LESENI YA MWENYE ALIYOPEWA NA JAJI MKUU WA KENYA

PROFESA WA AMERIKA AMTAMBUA MWENYE

Mnamo mwaka wa 1987 kulingana na kalenda ya kizungu, Profesa wa kizungu akiitwa Mr Marc J. Swartz kutoka chuo kikuu cha California San Diego (University of California,San Diego) alikuja mombasa kwa mas'ala ya kufanya utafiti (Research). Bwana huyu kwa bahati nzuri akapatana na Mwenye Karama na akaweza kumfanyia majaribio (Interview) na haswa katika mas'ala ya Tiba. Baada ya hapo yule Profesa akafurahishwa sana na ujuzi wake mpaka akamuandikia barua ya utambuzi (recognition letter) akisema "huyu ambae nimemuandikia barua hii ni mtu ambae ni msomi daraja ya mwisho (he is extremely learned) na anayo ilimu ya hali ya juu sana".

Barua aliyoiandika Professor Marc .J. Swartz kwa kizungu hii hapa nimenukuu:

"During June and July of this Year, I had the good fortune to discuss with Shariff Muhammad Hassan ("Mwenye Karama") various aspects of Medical practice and Human physiology. Shariff Muhammad was both extremely knowledgable and very generous in talking with me and my understanding of medicine and how the body works was greatly advanced as a result of the information and experience he shared with me. I am much indebted to "Mwenye" and I would like it generally known that he is a gentleman and a scholar of the highest quality.

The hospitality and kindness that have been accorded to me by the people of Mombasa has been a source of great help to me and none has been of greater assistance than

Shariff Muhammad Hassan Ahmed. This public acknowledgement of his generous assistance is a small token of my gratitude to him." Mwisho Wa Nukuu

UNIVERSITY OF CALIFORNIA, SAN DIEGO

BERKELEY • DAVIS • IRVINE • LOS ANGELES • RIVERSIDE • SAN DIEGO • SAN FRANCISCO SANTA BARBARA • SANTA CRUZ

DEPARTMENT OF ANTHROPOLOGY LA JOLLA, CALIFORNIA 92093

27 July 1987

To Whom It May Concern:

During June and July of this year I had the good fortune to discuss with Shariff Mohamed Hassan Akhmed ("Mwenye Karama") various aspects of medical practise and human physiology.

Shariff Mohamed was both extremely knowledgable and very patient in talking with me and my understanding of medicine and how the body works was greatly advanced as a result of the information and experience he shared with me.

I am much indepted to "Mwenye" and I would like it generally known that he is a gentleman and a scholar of the highest quality.

The hospitality and kindness that have been accorded to me by the people of Mombasa has been a source of great help to me and none has been of greater assistance than Shariff Mohamed Hassan Akhmed.

This public acknowledgement of his generous assistance is a small token of my gratitude to him.

Sincerely yours,

Marc J. [illegible]

Marc J. [illegible]
Profe[illegible]

KUSOMESHA

Mwenye Karama alikuwa ni mtu mnyenyekevu,mkarimu na mwenye hima katika mambo ya kheri, alikuwa ni mtu mwenye msimamo wa kudumu katika ratiba zake daiman bila kubadili misimamo yake katika mambo ya faida kwa Ummah,na bidii hizi na mudaawama huu aliweza kufundisha na kutoa natija nzuri sana katika wanafunzi, na amesomesha wengi sana tangu awamu yake ya kwanza hadi pumzi yake ya mwisho,na alikuwa husomesha Msikiti au nyumbani kwake, kwa kuwa hakuwa na Madrasa rasmi na akisomesha pamoja na uzee wake au ugonjwa wake.

Mwenye akisomesha darasa nyumbani baadal asri

Mwenye Karama hakuchagua wala hakubagua wanafunzi wake. Ilikuwa mwezi wa Ramadhani yeye ndiye huendesha darasa kubwa ya tafsirul Qur'an mjini Mombasa.

Alikuwa na bidii ya hali ya mwisho katika kusomesha, ikafika hadi akawa anasomesha mpaka taa zikizima msikitini huku akitumia tochi kusomeshea.

Mwenye Karama akisomesha darasa Masjid Noor Baada ya Swala ya Al-Fajiri

SUBUH
JUMAA
FAJRI
ZUHUR
ASHAR
MAGHRIB
ISHAI
ILANI

Wanafunzi wake wa Mwenye Karama waliokuwa wakihudhuria **darasa ya Masjid Noor (Bondeni)** alfajiri;

1. Al Habib Muhammad Mustafa Abu Numay
2. Sayyid Athman Umar Abdallah Saggaf
3. Ustadh Omar Abubakar Omar
4. Sheikh Muhammad Abubakar Omar
5. Ustadh Ali Nassor Said (R.A)
6. Sheikh Masud Idarus
7. Sheikh Ali Abdallah
8. Sheikh Abdulrahman Mukhtar bin Ibrahim
9. Ustadh Badru Khamis
10. Sheikh Abud Muhammad Ali Al-Famawy
11. Sayyid Muhdhar Khitamy
12. Ustadh Abdulrazaq bin Saleh
13. Sayyid Umar b. Abdallah b. Athman Saggaf
14. Ustadh Ashbal Karama
15. Ustadh Umar bin Ahmad
16. Sayyid Dr Adnan Maulana Al-Ahdaly
17. Sayyid Adnan Mudhhir Maulana Al-Ahdaly
18. Sheikh Abdulrahim bin Muhammad bin Ali Almaawy
19. Sayyid Abdallah bin Ahmad Alwarith
20. Sheikh Fakhi Yaasin
21. Sharif Omar bin Abraar AlNadhiry
22. Sharif Abubakar bin Abraar Al Nadhiry
23. Sharif Abdalla Mudhhir Qullatein Al-Nadhiry
24. Sheikh Ali Abdulqadir (Jilany) Al-Barawy
25. Sheikh Abud Muhammad Al-Shirazy
26. Yaakub Abdulhamid Sheikh

Mwenye Karama akisomesha darasa Masjid Anisa kabla ya Swala ya Adhuhuri

Mwenye Karama akisomesha Darasa ya Masjid Azhar (Baghani) baada swala ya magharibi

Mashekhe waliokuwa wakihudhuria darsa ya masjid azhar

1. Sheikh Ali Mwinzagu
2. Sheikh Ali Swaleh
3. Sheikh Muhammad Al-Haady
4. Sayyid Muhammad Hassan Al-Habshy
5. Sheikh Muhammad bin Ali Mwinzagu
6. Sheikh Muhammad Muhsin
7. Sheikh Kombo bin Haji Mshenga
8. Ustadh Ibrahim bin Ali



Mwenye akitwalii darasa ya Magharibi kabla ya kutoka kwenda mskiti wa azhar. Alikuwa akitoka kwa miguu kuelekea mskitini saa kumi na moja.

UNDUGU NA URAFIKI NA HABIB AHMAD MASH-HUR BIN TWAHA AL-HADDAD

Al-Habib Ahmad Mash'hur bin Twaha Al-Hadad ni katika waalimu wakubwa wa Mwenye Karama.
Al-Habib Ahmad alikuwa akiswalisha Swala ya Tarawehe katika Msikiti wa Birikao pale Bondeni na baada ya Swala kumalizika, alikuwa akitoa mawaidha kidogo na Mwenye Karama ndiye aliyekuwa akifasiri darsa hiyo kwa lugha ya Kiswahili. Baada ya Al-Habib Ahmad Mash-hur bin Twaha Al-Hadad kusafiri kuelekea Jeddah, Mwenye Karama ndiye alishika maqam hayo na akaendelea na Swala ile ya Tarawehe pamoja na darasa ile.

IJAZA YA MWENYE ALIYOPEWA NA AL-HABIB AHMAD

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله خالق الحب والنوى ممسك الطير في الهوا

فاتق رتق المعميات فتكون واضحة سوى

نسأله الزيد من جوده والطانية من شهوده،

وكمال الاقتداء بحبيبه خير عبيده محمد بن عبد الله

صلى الله عليه وعلى آله وصحبه ومن والاه،

وبعد فقد التمس مني الاخ الفاضل محمد بن حسن النضري العلوي

الاجازة المعهودة بين ذوي الرواية والدراية من

اهل العلم والرعاية ليتلقونها خلفاً عن سلف فتجمعهم

دائرتها على الانتظام في خير صف اما مهم فيها زين الوجود

والرحمة المهداة لكل موجود صلى الله عليه وعلى آله وصلوا بحضرته واستمسكوا

بعروته بواسطة سمط الاجازة المنظود

ولأجل المساهمة في نيل الجواز على مجاز تلك الاجازة،

والفوز بقطع مهول تلك المفازة أجبت اخي المذكور

مراجزته لفظا وكتابة فيما تصح لي فيه الاجازة من علوم

واعمال واوراد واذكار وسلوك وطريقة كما تلقيتها

سماعا وبالواسطة عن مشائخي الاعلام

وفي مقدمتهم سيدي الغوث صالح بن عبد الله الحداد والحبيب صالح بن عبد الله
وعمامي العلمين الشريفين عبد الله وعلوي ابنيه الحداد
ووالدي النسيب طه بن علي الحداد ومن الشيخ البركة
عمر باطوق العمودي وسيدي الإمام الكريم
مصطفى بن أحمد المحضار والحبيب العلامة عمر بن أحمد الهدار
ومن تريم) الحبيب عبد الله بن عيدروس العيدروس والحبيب العارف
عبد الباري بن الشيخ العيدروس والحبيب الإمام عبد الله بن محمد الشاطري
والحبيب العلامة علوي بن عبد الله بن شهاب؟
(ومن سيون) الحبيب العارف أحمد بن عبد الرحمن السقاف والحبيب
العلامة محمد بن هادي السقاف والحبيب محمد بن علي الحبشي
(ومن الحريضة) الشيخ العلامة عمر بن عبيد باجنيد والسيد العلامة
عيدروس بن سالم البار والسيد الحبر العلامة الشريف أحمد الشاطري
والسيد العلامة محمد عبد الحي الكتاني
(ومن حاوي) الحبيب العلامة محمد بن أحمد المحضار
عبد الله بن محسن العطاس والإمام الحبيب علوي بن عبد الله
علي بن عبد الرحمن الحبشي والحبيب العارف بالله أبو بكر بن محمد السقاف
(ومن أريقيا) الحبيب العارف بالإمام صالح بن علوي جمل الليل
وآخر من أخذت عنه الحبيب الإمام عمر بن أحمد بن سومل
فقد ظفرت والحمد لله من بحر الإمداد الإلهي وغيرهم

ممن لهم ذكرهم بالاخذ والاجازة والاقراء
لفظا وكتابة في علوم الكتاب والسنة والاصلين
وكتب القوم وحزبهم بحسب تراجمهم واسانيدهم
الملتقية على اثباتهم المشهورة والاسانيد الخطية ومن اجلتها
عقود اللآلئ وعقد اليواقيت للحبيب الامام المجاهد
عبد الرحمن بن عمر الحبشي وصحة الآلاء الغافر للحبيب العلامة
سالم بن حفيظ بن الشيخ ابي بكر بن سالم وما اشتمل عليه
كتاب المواهب والمنن للحبيب العلامة احمد بن حسن الحداد
وقرة النواظر لسيدي العلامة عبد الله بن طاهر الحداد
والشبت الجامع لسيدي العلامة علوي بن طاهر الحداد
وفيض الاسرار للشيخ العلامة عبد الله بن احمد باسودان
وما ارويه عن مشائخي بما يروون عن الامام المجاهد
الكبير احمد بن حسن العطاس من اسناد وثبت عن
ما يرويه واتصلت به من اسناد عن الحبر الجامع والبحر الواسع
الحبيب عبد الله بن علوي الحداد

وقد اجزتنا في المذكور بما اجازني به هؤلاء الاعلام
فاوصيك بتقوى الله في السر والعلانية والتواضع
في القول والفعل والصدق في الجد والهزل

والتقصد في الغنى والفقر (التواضع) والاقبال على
طلب العلم بجد وتشمير وحسن الظن في الصغير والكبير
واغتنام الخمس والمحافظة على الخمس والاتباع للمخصوص
بالخمس ونشر دعوته ودينه في امة الأئمة والأجابر؛
وتقريبهم الى الله، وان لا ينساني من دعائه
ولاحبابه كمال النجح والاستقامة والفتح والكرامة
بحق محمد وآله صلى الله عليه وعليهم وسلم

وكتبه بيده الفقير الى الله
احمد مشهور طه الحداد

الجمعة ٢٣ ذي القعدة ١٤٢٨ هـ
الموافق ٨/٧/٢٠٠٨ م

BAADHI YA SIFA ZAKE TUKUFU

Mwenye Karama alikuwa Mcha-Mng'u wa kupigiwa mfano. Sifa hii ya Ucha-Mungu wake walikubaliana watu wote watukufu wa zama zake. Na mwenye kumcha Mwenye-Ezzi-Mng'u, kila kitu humuogopa!

Alisifika kwa ukarimu wa hali ya juu. Katika ada yake kila siku, baada kuswali alfajiri, atoke hapo nje ya msikiti noor atoe sadaqa kwa maskini walokuwa hapo. Alikuwa haogopi ufukara, akitoa mali yake kwa wajane na maskini kila siku.

Alikuwa ni mtu mpole na tena ana tawadhui. Akipiga goti mbele ya mmoja wa wanafunzi wake ili kusoma kwake.

Alikuwa na himma kubwa ya kusomesha watu na akifanya dhihaka na wanafunzi wake.

Alikuwa akiwalea na kuwatizama watoto wake wa kambo kama kwamba ni watoto wake binafsi.

KUSIFIWA NA MWANACHUONI MWENZAKE

Ustadh Harith Swaleh alimsifu kwa kusema, “Huyu bwana, muoneni kwa haya macho nitakayo waambiya, aliketi akashika zuo mbee ya shekhe lake tangu yungali kijana, mpaka na shekhe yuwamuambia wasomeshe hawa. Na mpaka ikaja siku ikawa shekhe hawezi kusomesha akawa yeye husomesha na shekhe yuko. Ikaja siku shekhe akakosekana duniani ikawa mahali pake ni mskiti wa azhar wa kibokoni. Huku ndiko kusuluhia wanangu!”

MWENYE AKIMZURU SHEKHE LAKE, MWENYE MUADH'AM



KUAGA DUNIA

Sayyid Muhammad bin Hassan (Mwenye Karama) aliugua akiwa nyumbani kwake, na maradhi yalipozidi alipelekwa Hosipitali ya Pandya, Mombasa na akalazwa hapo siku chache kabla kufariki.

Mwenye Karama aliitikia wito wa Mola wake magharibi ya kuamkia Jumapili tarehe 25 Shaaban 1441H, sawia na tarehe 18 April 2020 CE, akiwa na umri wa miaka 83.

Waliyemuosha na kumzika ni;

1. Sayyid Abdulqadir (Jeilani) (mtoto wake)
2. Sayyid Muhammad Abdulhalim (mjukuu wake)
3. Adnan Maulana Al-Ahdaly (mwanafunzi wake)
4. Yaakub Abdulhamid (mwanafunzi wake)

Mwenye Karama alizikwa katika Maziyara ya Kikowani upande wa Seif Halwa pambizoni mwa shekhe lake, Sharif Muadham bin Amin Al-Rudainy.

Mwenye alifariki katika kipindi kigumu cha janga la ugonjwa wa Virusi vya Korona, ikawa ni vigumu watu kujitokeza kuja kumzika kigogo huyu kwani Serikali ilikuwa imesitisha mikusanyiko ya watu na pia kulikuwa kumewekwa idadi maalum ya wenye kuhudhuria Mazishi.

Haya ndiyo maisha ya Mwenye Karama kwa mukhtasari. Twamuomba Mola Subhanahu wa Ta'ala atunufaishe

kwa baraka za bwana huyu na atufungamanishe na watu wema hapa duniani na kesho aakhira. Amfinike kwa Rehma zake tukufu, na amlipe majazi mema kwa kazi kubwa alioifanya na atujaalie sisi ni wenye kufuata nyayo zake. Amin

Na rehma za Mwenye-Ezzi-Mng'u zimfikie Bwana wetu Muhammad pamoja na Aali zake na Swahaba zake. Amin

MIRTHAAT ALOTUNGIWA MWENYE KARAMA R.A

Hii imetungwa na mwanafunzi wake;
Sayyid Umar bin Muhammad bin Abraar Al-Nadhiry Hafidhahullah

بسم الله الرحمن الرحيم

QASIDA YA KUMUELEZA AS-SAYYID MUHAMMAD BIN HASAN AN-NADHIRY (MWENYE KARAMAA)

أَحِلَّ رِضَاكَ رَبِّي وَٱلسَّلَامَا ۞ عَلَىٰ مُحْيِي الْهُدَى مَيْنَيِ كَرَامَا

وَجُدْ صَبْرًا لِمَنْ صَارُوا حُيَارَىٰ ۞ وَأَصْبَحَ يَوْمُهُمْ لَيْلًا تَمَامَا

وَغَشَّاهُمْ مَصَائِبُ لَوْ أُفِيْضَتْ ۞ عَلَى جَبَلٍ لَذَابَ وَمَا أَقَامَا

وَظَلُّوْا كَالسُّكَارَى فَقْدَ حِبٍّ ۞ بِمَوْتِهِ عَمَّتِ الدُّنْيَا ظَلَامَا

فَقِيْهٌ قَامَ يَدْعُوْ النَّاسَ حُبًّا ۞ إِلَى الْمَوْلَى عَلَى الصِّدْقِ اسْتَدَامَا

وَيُنْفِقُ بَعْدَ كُلِّ صَلَاةِ فَجْرٍ ۞ نُقُوْدًا لِلْأَرَامِلِ وَٱلْأَيَامَىٰ

فَيَقْرَأُ وَٱلْمُحِبِّيْنَ الْقُرَانَ الْ ۞ مَجِيْدَ رِضًا لِمَوْلَاهُمْ سَلَامَا

فَيَنْشُرُ فِيْهِمُ أَنْوَارَ عِلْم ۞ يُزَكِّيْهِمْ وَيُعْلِيْهِمْ مَقَامَا

فَيَقْتَبِسُ الْفُيُوْضَاتِ الْإِلَهِ ۞ يَّةِ الْعُلْيَا جَلِيْسُهُ وَٱلْمَرَامَا

يُصَلِّي بَعْدُ رَكْعَاتٍ ثَمَانٍ ۞ صَلَاةَ ضُحًى يُزَيِّنُهَا تَمَامَا

حَوَى خُلُقًا كَرِيْمًا وَٱسْتَنَارَتْ ۞ جِهَاتُ بِلَادِنَا بِهِ يَا نَدَامَى

وَفَـاقَ الدَّهْـرَ بِـالْـهِـمَـمِ الْـعَـوَالِي ۞ وَجَـادَ الْخَـيْرَ مُـتَّـبِـعًـا كِـرَامَـا

وَكَانَ مُـوَاسِـيًـا ضُـعَـفَـاءَ مِـنَّـا ۞ وَيُـبْرِئُ مَنْ أَتَوْا وَجْعَى سِـقَامَا

وَيُـوْدِعُ أَطْيَـبَ الْأَخْبَـارِ أَسْـمَـا ۞ عَـهُـمْ طَوْعًا وَيَجْتَنِـبُ الْمَـلَامَـا

وَيَـغْـمُـرُ قَـاصِـدِيْـهِ بِتَـمِّ لُـطْفٍ ۞ وَيُـوْلِي صَـحْـبَـهُ بِـرًّا تَـنَـامَى

وَيَـرْعَاهُـمْ وَيَحْـتَـمِـلُ الْـمَشَـقَّـا ۞ تِ فِي تَعْلِيْمِهِمْ كُتُـبَ الْقُدَامَى

يُؤَلِّـفُ بَيْنَهُمْ فَرِحًا وَيَكْسُـو ۞ هُـمُ حُـلَـلَ السَّـعَـادَةِ ذَا أَدَامَـا

وَيُـتْـحِـفُـهُـمْ ذُرَى الْبَرَكَاتِ رَفْـعَـا ۞ ظَـرَافَـتَـهُـمْ وَيَـزْدَادُوْا الـتِزَامَـا

وَيَسْـأَلُنَـا عَـنِ الْأَحْبَـابِ مَـا فِي ۞ هِمُ يَتَفَقَّدُ الصَّـحْبَ الْحِشَـامَا

يَصُـوْنُ لِسَـانَـهُ إِلَّا بِخَـيْرٍ ۞ وَيَمْشِـي الْهَوْنَ مُلْتَمِسًا سَلَامَا

وَرُأْيَـتُـهُ تُـزِيْـلُ الْـغَـمَّ عَـنَّـا ۞ وَتُحْـيِـيْـنَـا وَتَجْـنُـبُـنَـا الْحَـرَامَـا

وَقُـرْبُـهُ قُـرْبُ خَـيْرَاتٍ وَمَـغْـنَـا ۞ هُ أَنْوَارٌ تُـغَـذِّي الْمُسْـتَـهَـامَـا

بِـهِ كَمْ فَاسِـقٍ أَمْسَـى تَقِيًّا ۞ وَذِي جَهْلٍ عَلَى الْعِلْمِ اسْـتَقَـامَـا

لَهُ سِـــعَـةُ الـرِّوَايَـةِ وَاطِّـلَاعٍ ۞ جَوَاهِرَ تَـنْفَحُ الـظَّمِـأَ الْمَـرَامَـا

بُـــرُوْعُهُ فِي الدِّرَايَةِ وَاضِـحٌ كَ الْ ۞ ذُّكَاءِ وَلَـمْ يَـزَلْ يُـوْفِي الذِّمَـامَـا

تَـلَـقَّى الْـعِـلْـمَ مِـنْ قَـوْمٍ ثِـقَـاةٍ ۞ هَـدَوْا خَلقًا إِلَى الْمُحْيِي عِظَامَـا

حَـوَوْا عِـلْـمًـا لَدُنِّـيًّـا عَـظِـيْـمَـا ۞ فَفَـاقُوْا وَاعْتَلَوْا نِعَمًا جِسَـــامَـا

كَسَـــادَتِـنَـا مُـعَـظَّـمِ الـرُّدَيْـنِيِّ ۞ عَالِي الْـقَـدْرِ وَالـزُّهـدِ الْإِمَـامَـا

وَنَـافِـحِـهِ فُـتُـوحَ الْـعِـلْـمِ طُـرًّا ۞ مُحَـمَّـدٍ الَذِي رَبَّى الْـعِـظَـامَـا

فَـذَا لِـكُـمُ الْبَرَيْـكِـيُّ الـظَّـرِيْـفُ ۞ الصَّـفِيُّ الْقَلْبِ عَنْ دَرَنٍ تَسَـامَى

وَمَـنْ بَـلَـغَ الذُّرَى فِي كُلِّ فَـنٍّ ۞ عَلِيٍّ مُـتْـقِـنِ الْأَدَبِ الْـهُـمَـامَـا

وَقُطْـبِ الْكَوْنِ أَحْمَـدَ ذِي الْمَعَـالِي ۞ هُوَ الْمَشْـــهُوْرُ بِـالتَّقْوَى دَوَامَـا

بِـتَـعْـظِـيْـمٍ وَحُـبٍّ وَاحْـتِرَامِ ۞ لَهُمْ نَـالَ الْمُنَى فَعَلَا مَـــقَـامَـا

فَكَانَ شَـــكُوْرَ مَوْلَاهُ صَـــدُوْقَـا ۞ وَضِيْئَ الوَجْهِ لِـــلتَّقْوَى لِزَامَـــا

كَـثِـيْرَ قِـرَاءَةِ الْـقُـرْآنِ ذِكْـرَا ۞ لِـرَبِّـهِ زَاهِـدًا دُنْـيَـا تَـمَـامَـا

عَـظِـيْـمَ الْحَـالِ مَحْـفُـوْظًـا ظَـهِـيْرَا ۞ أُمُـوْرَ الْخَـيْرِ مُجْـتَـنِـبًـا حُـطَـامَـا

طَلِيْقَ الْوَجْـهِ مُشْـــــرِقَـهُ مَهِيْبَـا ۞ وَقُـوْرًا ذَا رُوَا فَـاقَ الْـوِسَـــامَـا

قَضَـــــى أَوْقَاتَهُ فِي نَشْـــــرِ عِلْمِ ۞ وَأَذْكَارٍ وَتَـطْـبِـيْـبٍ سِـــقَـامَـا

سَـــقَـانَا مَا سَـــقَـانَا مِنْ كُؤُوْسِ الْ ۞ وُصُـــوْلِ إِلَى رِضَـــا الْهَادِي الْأَنَامَا

مُـنَـجِّي مَـنْ أَحَـاطَ بِـهِ كُـرُوبٌ ۞ وَنَـادَى يَـا مُشَـــفَّعَنَـا سَـــلَامَـا

إِلَى الْـــــمَوْلَى تَوَسَّـــلْنَـا رَحِيْمَ الْ ۞ وَرَى بِكَ كَيْ يُوَافِيَنَا الْـــمَرَامَـــا

فَقُمْ وَأَغِثْ وَأَكْرِمْ مَنْ دَعَـــوْكَ الْ ۞ رِّضَى وَالنَّصْـــــرَ واعْطِهِمُ وِئَامَا

عَـلَـيْـكَ صَـــلَاةُ رَبِّي يَـا طَـبِـيْـبِي ۞ وَتَسْـــلِـيْـمَـاتُـهُ تَـتْرَى دَوَامَـا

كَـذَا الآلُ الَّذِيْـنَ حُـبُـوا نَـقَـاءَ ۞ وَمَنْ صَـحِبُوْا مُصَـحِّحَنَا العِظَامَا

وَذُوْ الحُسْـــنَى مُحَـمَّـدُ الْـمُـعَـلَّ ۞ الَّذِي أَحْيَى الهُـدَى مَيْنَيْ كَرَامَـا

مَتَى نَـــادَى ذَوُوْ صِدْقٍ عَلَيْـــهِمْ ۞ أَحِـلَّ رِضَـــاكَ رَبِّي وَالسَّـــلَامَـا

بسم الله الرحمن الرحيم

قصيدة في رثاء بقية السلف العارف بالله تعالى العلامة الفقيه النحوي الطبيب

الحبيب محمد بن حسن النضيري العلوي الحسيني

الملقب بـ (منيه كرامه)

نَصَرَ الشريعةَ رافعًا إسلامَهْ ... شيخُ الشيوخِ العارفُ العلاّمَهْ

جَمُّ الكرامة فَيلَقٌ مُتبحّرٌ ... مَن ذا يساهمُ بعدهُ إسهامَهْ

ليس الكرامةُ أن تطيرَ على الهَوَا ... إنّ الكرامة أنْ تكون (كرامَهْ)

فَقدتْ سواحلُنا فقيهاً بارعاً ... فالعِلمُ غيثٌ والفَقِيدُ غمامَهْ

شهدتْ له جُلُّ المساجدَ عاكفاً ... للشرعِ يُوْضِحُ حِلَّه وَحَرامَهْ

أو درسِ تفسيرٍ وعِلْمِ تصوّفٍ ... ما كان إلا قُدوةً فَهّامَهْ

وله مع التدريس نورُ عبادةٍ ... في وجهه الميمُونِ كان وِسامَهْ

ألقى عليه جلالةً ومهابةً ... مولاهُ فازدادَ الحبيبُ وَسامَهْ

ما كان ثَرثَاراً يُمِلُّ جَليسَه ... بل كان مقتصداً يَكِيلُ كلامَهْ

أحيي الطريقةَ في سلوكٍ باهرٍ ... فهو الشريفُ عمامةً وإمامَهْ

ما خاض في ذَمٍّ ولا ذَمٍّ ولا ... جدلٍ عقيمٍ ليس فيه سلامَهْ

زانته أخلاقُ الرسول مبكّراً ... والله يُولي عبده إنعامَهْ

تلك العنايات التي إن لاحظتْ ... قلباً سقته من اللباب مُدامَهْ

من نسل أطهارٍ وبيت فتوّةٍ ... آل النضيريْ أسوةٌ وزعامَهْ

ربّاه فَاجْبُرْ كسرَنا بمُصابهِ ... والطف به في برزخٍ وقيامَهْ

ألهِمْ ذَوِيهِ الصبرَ واجمع شملهمْ ... واحفظ لهم بعد الفقيد مقامَهْ

ثم الصلاة على النبي وآله ... ما نَاحَ يوم البين صوت حمامَهْ

شعر السيد صالح الأهدل

توفي الإمام العلامة مساء الأحد ٢٥ شعبان ١٤٤١هـ الموافق ١٩ ابريل ٢٠٢٠م

رحمه الله تعالى رحمة الأبرار وأسكنه جنات تجري من تحتها الأنهار، وجعله مع النبيين والصديقين والشهداء والصالحين، ورحمنا والأمة به، إنه أكرم الأكرمين

Marejeo ya Vitabu niliyotumia

1. Sharif Aidarus b. Ali Al-Nadhir, Al-Badrul Munir fi Nasab Saada Aal Nadhir

2. Sharif Aidarus b. Ali Al-Nadhir, Bughyatul Aamal fi Tarikh Soomal

3. Sayyid Muhammad b. Ahmad b. Umar Al-Shatry, Al-Mu'jamul Latwif (Uk 179)

4. Sayyid Abdulrahman b. Muhammad Mash-hur, Shamsu Dhwahira (Uk 566)

5. Amir Shakib Arslan, Hadhirul Aalam Al-Islaamy (Mj. 3 Uk 182)

6. Al-Habib Ahmad b. Abubakar b. Sumayt, Tuhfatul Labib (Uk 132)

7. Ustadh Harith Swaleh, Chaguo la Wanavyuoni (Uk. 38-39)

8. Al-Habib Abdulqadir bin Abdulrahman Al-Juneid, Al-Islam Wal Yamaaniyun Al-Hadharim bi-sharq Afrikiya (Uk 40-41)

9. Sheikh Mustwafa Iqbal Sameja, Ladhatun Li Sharibiin fi Tarjuma Khalifatul Qadiriyya, Al-Habib Umar b. Muhammad Qullatein

10. Sayyid Abdulqadir Juneyd, Al-Islam wal Yamaniyyun Al-Hadharim fi Sharq Afrikiya (Uk 42-44)

Waliochangia kupitia njia ya Mahojiano

1. Sayyid Hassan bin Muhammad Al-Nadhiry
2. Sharif Omar Ali Al-Nadhiry
3. Ustadh Abdulrazaq Saleh
4. Sayyid Athman bin Abdallah Saggaf
5. Ustadh Abud Muhammad Ali Al-Famawy
6. Sayyid Umar bin Muhammad Abrar Al-Nadhiry
7. Ustadh Ashbal Karama
8. Sayyid Muhammad Bahsan Noor Al-Nadhiry